Kiswahili is undoubtedly one of the most developed and expansively used indigenous African languages nationally and internationally. Currently, Kiswahili is one of the most taught languages globally. Many international Universities in Europe, Asia, America, and Africa have Kiswahili as one of the African languages in their curricula (Amidu, 1995; Mulokozi, 2002; Okombo and Muna, 2017). For example, in America and Europe, more than 200 universities teach Kiswahili (Okombo and Muna, 2017). This article aims at assessing the teaching of Kiswahili as a foreign language in Germany. Specifically, the article aims at identifying stages in which Kiswahili is taught, challenges, success, solutions and available opportunities. Two Universities; University of Leipzig and University of Bayreuth will be used as case study. Data will be obtained using interview with swahili instructors and students who learn swahili in various stages. The article is expected to add knowledge in the field of Second/foreign language teaching and learning

14. Dyoniz Kindata (Lueneburg)

Genre Developments in the Colonial Kiongozi Newspaper in German East Africa 1885-1918

In this presentation, I would like to present the results of the third chapter of my dissertation which deals with the genre, layout and format of the Kiongozi. My dissertation is entitled "Poetic and Photographic Practices in the Kiongozi Newspaper in German East Africa 1885-1918". Therefore, the aim of this article is twofold: First, to demonstrate how the genres of the Kiongozi newspapers have evolved over the years, especially the literary genres. Secondly, to show the layout and formats of the newspaper, while also investigating and/or questioning the notion of readership, editorship, authorship and censorship in the newspaper.

15. Ahmed Kipacha (Arusha)

Mabadiliko ya Kitahajia ya Kiswahili: Ushahidi wa Kiswahili cha Kati katika Mamboleo na Uwongozi

Je, upo uwezekano wa lugha ya Kiswahili kubainishwa kiwakati katika vipindi vya awali, vya kati na sasa? Makala hii ni mapendekezo ya uwezekano huo. Tangu kupatikana kwa teknolojia ya hati za Kiarabu na Kirumi katika ukanda wa Kiswahili, tunauhifadhi wa kimaandishi wa lugha ya Kiswahili katika vipindi mbalimbali vinayoashiria mabadiliko ya kisarufi, kisauti na kitahajia. Makala hii inapendekeza kupitia ubainishaji wa historia ya usanifishaji wa Kiswahili wa Ileri Mbaabu (1991) kuwa kipindi cha kuanzia 1930 ambapo usimikwaji wa kanuni za usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili ulianza ni Kipindi cha Muhula wa Sasa (KMS). Kabla ya hapo ni Kipindi cha Muhula wa Kati (KMK). Kipindi cha Muhula wa Awali (KMA) ni kabla ya maandishi ya hati za Kiarabu katika karne ya 12. Kwa kuanzia, hoja inajengwa juu ya uwepo wa Kiswahili cha Kati kupitia ushahidi wa kitahajia katika ngazi ya kiisimu. Tutarejelea magazeti ya *Mamboleo* (1923-1925) na *Uwongozi* (1930-1932). Tahajia katika magazeti hayo inalinganishwa na ushahidi wa kitahajia unaopatikana katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) ikiwa ni ushahidi wa data ya kitahajia ya Kiswahili cha sasa. Hii ni hatua ya awali katika ukusanyaji wa ushahidi wa mabadiliko ya lugha ya Kiswahili katika vipindi mbalimbali. Bado kunahitajika utafiti zaidi wa maandishi ya Kiswahili katika ngazi za kileksika, kisémantiki, kifonolojia, na kimofosintaksia, kupitia nyaraka za kiserikali, matini za kifasihi, barua za watu binafsi, vitabu vya kitaaluma, misahafu ya kidini, na maandiko ya kiakiolojia kabla ya 1930 ili kujenga picha kamili ya mabadiliko ya Kiswahili katika ngazi mbalimbali.

16. Ma Jun (Shanghai)

“中体西用” in Eastern Africa: Reflection on the Research Path of Modern Swahili Studies with the Historical Experience of East Asia

At the end of the 19th, when the Anglo-French coalition forces and the American black ships brought modern Western culture to East Asia along with the flames of war, the ancient East Asian countries adopted an eclectic approach to accepting these values that were utterly different from their traditions. Furthermore, as far as possible to ensure its subjectivity, thus began the construction and development of the modern nation-state. People in China call it “中体西用 (zhōng tǐ xī yòng): *Chinese Body and Western Function*,” and people in Japan call it “和魂洋才 (わこんようさい): *Japanese Spirit and Western Talent*.” Its core idea is based on the country’s traditional morality, values, culture, and political system while introducing as much Western science and technology as possible. This method fully retains the traditions of these countries from the institutional level, and while introducing science and technology, it also introduces Western humanistic ideas. From the perspective of historical development, the idea of the “Chinese Body and Western Function” as an example was a kind of active response to the impact of Western humanistic thought by the disadvantaged East Asian countries at that time. It is generally believed that this is of great significance for East Asian countries to maintain their own cultural subjectivity. A century later, the global flow of knowledge has not changed much, and Western thought remains in a relatively strong position. Under such circumstances, how can the southern countries ensure their intellectual subjectivity? Let us go a step further and discuss how the native knowledge experience of Africa, taking Swahili as an example, ensures its subjectivity in the global knowledge flow while at the same time absorbing and learning as much knowledge from the outside world as possible. This paper hopes to provide a new possibility for the research path of Modern Swahili Studies by discussing the historical experience of East Asia.

17. Vincent Magugu (Eldoret)

Mwangwi wa Utu Katika Fasihi ya Kiswahili

Bara la Afrika limewahi kurejelewa kama ‘Bara la giza’ kutokana na uchukulio wa kimsingi kwamba Wafrika walipungukiwa katika ngazi zote za maisha na walihitaji kustaarabishwa. Matokeo ya uchukulio huu yalikuwa ni mvurugiko wa asasi za kiasili katika jamii za Kiafrika pamoja na mkengeuko ambao umezaa utegemezi unaoshuhudiwa sasa. Licha ya uchukulio huu potovu, kuna dhana za kiasili ambazo zimedhihirishwa kuwa zenye uwezo mkubwa wa kuzielekeza jumuiya za Afrika na kuziwezesha kukabiliana na changamoto za kisasa. Hata hivyo, kutokana na athari za ukoloni na mkengeuko uliopo barani Afrika, dhana hizi zinatuhitaji kutafakari upya ukombozi wa Mwafrika hasa tukirejelea falsafa kama msingi wa ukombozi kamili huu. Utu, kama falsafa, umeibuka kama mojawapo wa misingi asilia katika jamii za Kiafrika ikiwemo ile ya Waswahili. Ni dhana inayofumbata na kubainika katika hali za maisha ya Mwafrika kijamii, kiuchumi, na hata kisiasa. Makala hii imetali udhihirikaji wa dhana na falsafa ya utu kama dira katika fasihi ya Kiswahili. Katika kufanya hivi, Makala imetathmini udhihirikaji wa mihimili ya kimsingi ya utu katika diwani ya *Mchezo wa Karata* iliyoandikwa na Kithaka wa Mberia. Ufafanuzi wa utu umejikita kwa kiasi kikubwa kwa ubainishaji uliotolewa na Kresse kutokana na uchanganuzi wake wa utenzi wa *Mtu ni Utu* uliotungwa na Ahmad Nassir. Makala imeangazia migogoro katika diwani ya *Mchezo wa Karata* inavyojengeka na kutatuliwa kwa msingi wa utu. Utafiti umefuata mwelekeo wa uzingatiaji wa mantiki kupata wazo la jumla katika kubainisha, kueleza na kufikia mahitimisho kuhusu dhana ya utu na udhihirikaji wake katika diwani hii.

**18. Jasmine Mahazi, Rayya Timammy & Rukiya Swaleh
(Berlin, Nairobi & Kilifi)**

**More than Three Swahili Women
Zaidi ya Wanawake Watatu wa Kiswahili**

In this paper we present from our ongoing collaborative research on matrifocal Swahili knowledge practices, among which prominently feature ngoma dance and music performances, religious education and artisanal handicraft. We argue that Swahili Studies, which is rooted in Western thinking and knowledge tradition, fails to provide an adequate framework for Swahili epistemologies to unfold. In our research, we go beyond a patrifocal and literary approach towards Swahili knowledge production, in particular Swahili literary creation, and attempt to unearth the matri-philosophy that underlies the lives of Swahili-speaking peoples of the Western Indian Ocean (Swahili culture), with the aim to re-read Swahili “his-story” and to midwife the telling of Swahili “her-stories” through seeking viable research tools and terms. Through presenting examples of three female figures, we want to show how matrifocal knowledge practices manage to dis-personify, spread and multiply intangible and ephemeral knowledge content and create communities of practice (Wissensgemeinschaft), instead of culminating in one renowned knowledge expert, single author or immortal hero. And yet we begin this journey by presenting on the lives and works of three Swahili heroines: *ustadha* Twaiba, *maalima* Swafiya and *maLulu*.

19. Mbwarali Kame (Eldoret)

Ushairi wa Kiswahili Ulivyoenziwa na Ustadh Mahmoud Mau: Shujaa Mashuhuri wa Kisiwa cha Lamu

Ushairi wa Kiswahili umepata umaarufu mkubwa sana ulimwenguni hasa ikizingatiwa kuwa ni ushairi ulioimbwa na mashujaa waliokienzi Kiswahili na kukipa kipaumbele katika karne ya kumi na nane na ishirini, muandamo wa karne ya ishirini na moja. Ustadh Mahmoud alijulikana kama mtuzi mashuhuri ambaye ushahi wake haukupishana sana na tenzi za zamani ambazo aghalabu zilikita katika kutoa nasaha za kidini. Nasaha husika zilikitwa kwenye maandiko matakatifu ya Quran na Hadithi za Mtume Muhammad. Mau kama kawaida yake hakisita kukopa mtindo mashuhuri wa kuanza ushairi wake kwa kutaja jina la Mwenyezi Mungu kwa matamshi yale yale ya Kiarabu kama ilivyotangulizwa katika Mwanakupona na Al-inkishafi. Makala hii basi inaangazia kwa umakini historia fupi ya mashujaa wa Ushairi wa Kiswahili wa karne ya kumi na nane na tisa. Pia, itafafanua Historia ya Shujaa mashuhuri aliyetambulika kisiwani Lamu kama malenga Ustadh Mahmoud Mau. Aidha, makala, inafafanua mbinu anazozitumia katika utunzi wa ushairi wake.

20. Naoemi Nzilani Musembi (Bondo)

Fasihi za Kiitikadi na Mchango Wake Katika Jamii ya Sasa

Makala hii inadhamiria kuchunguza suala la itikadi katika riwaya ya G. K. Mkangi *Walenisi* (1995). Mojawapo ya dhana zinazopatikana sana katika uhakiki na uchambuzi wa fasihi ni itikadi. Itikadi hutazamwa kama mawazo au mwongozo wa kimawazo unaoudhibiti mkabala wa mwandishi kuhusiana na masuala mbalimbali. Riwaya ya *Walenisi* inajihusisha kwa kiasi kikubwa na suala la kisiasa. Ni riwaya ya kiitikadi na inaonyesha msimamo wa mwandishi Mkangi kuhusiana na masuala ya kijamii, kisiasa, kidini na kiuchumi. Inaiponda serikali ya Kenya kwa uozo uliokuwepo serikalini wakati akiitunga. Riwaya hii inaonyesha uovu uliopo katika tawala ambazo hazitilii maanani maslahi ya wengi. Katika fasihi za kiitikadi, mwandishi huwa na dhamira wazi ya kuendeleza mkondo Fulani wa uwazaji na wa kuifasiri tajriba yake. Anafanya hivyo kwa kuona mkondo fulani wa kimaisha kama unaofaa na labda kwa kiasi fulani anaupendekeza kwa wasomaji wake. Nia kuu ya makala hii ni kuonesha kuwa, ili kazi ya mwandishi fulani ieleweke bayana, ni muhimu kuelewa msimamo wake kuhusu masuala mbalimbali yanayoiathiri jamii yake. Hivyo basi, makala haya yanapania kuchunguza masuala ya kiitikadi aliyoyamulika Mkangi ili kuiponda udhairi unaowapotosha wanajamii kwa kuchukulia hali fulani kuwa kama dhahiri bila kutambua kuwa, msingi hasa ni itikadi ambayo inatawala. Mkangi alilenga kuwamulikia wasomaji wake kuhusu namna ambavyo itikadi ina uwezo wa kuwapofusha wasiitambue. Alijaribu kubadilisha jumla ya mawazo ambayo hudhibiti jinsi wanajamii wanavyoukabili, kuufasiri na kuuelewa ulimwengu wao. Makala hii itaongozwa na nadharia ya uyaakinifu wa kijamaa.

Istilahi Muhimu: Itikadi, Falsafa, Uozo

21. Asifiwe Eliud Mwangike (Dar es Salaam)

Utelezi wa Fanani na Hadhira Kwenye Utendaji wa Utani wa Msibani

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji, fanani ni mtu au kikundi cha watu wanaotenda kazi ya fasihi simulizi mbele ya hadhira huku wakijua kuwa kuna watu wanaowatazama na watu hao wanatoa tathimini ya utendaji wao (Bauman, 2012). Ili kufanikisha jambo hilo fanani hujiandaa na wakati mwingine hukariri baadhi ya vipengele vya kazi yake (Mulokozi, 2002). Mtazamo huu unaozichukulia nafasi za fanani na hadhira kama vipengele tofauti ndiyo uliozoeleka miongoni mwa wataalamu wa fasihi simulizi (taz. Okpewho, 1992; Finnegan, 2002 na Mulokozi, 2017). Kwa hiyo, dhana hizo zimekuwa zikijadiliwa kwa namna ambayo zinaonekana ni vipengele tofauti kabisa ilhali ni dhana ambazo wakati mwingine hakuna mpaka bayana unazozigawa. Kutokana na changamoto hiyo ndiyo maana Mnenuka (2020) anapendekeza dhana hizo zichunguzwe kupitia ugiligili wake na si utisiti. Makala hii inalenga kufafanua utelezi wa dhana ya fanani na hadhira wakati wa utendaji wa utani wa msibani kutoka katika jamii ya Wahehe nchini Tanzania. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kushuhudia misiba inayohusisha utendaji wa utani pamoja na kufanya mahojiano na fanani wa utani kutoka jamii hiyo. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba kuna unyumbufu wa fanani na hadhira, mpaka usio bayana baina yao na wakati mwingine fanani na hadhira kuwa kitu kimoja.

22. Mwalimu Deogratias Ngonyani (Michigan)

Simulizi za Marijani Rajabu katika Nyimbo Narratives in Marijani Rajabu's Songs

Mwimbaji Mtanzania, Marijani Rajabu (1955-1995), alijulikana sana wakati wa uhai wake kwa nyimbo zake tamu na hata wanamuziki wa kizazi cha sasa huiga na kuziimba nyimbo zake. Licha ya sanaa yake ya kimuziki, M. Rajabu ana mchango mkubwa katika matumizi ya lugha katika nyimbo zake. Mchango wa M. Rajabu katika kujieleza na kuelezea hisia juu ya masuala mbalimbali ya jamii, siasa, na hata mapenzi unahitaji kuchunguzwa. Makala hii inaangazia muundo wa nyimbo zake kwa kuzingatia mambo mawili: (a) ruwaza na usambamba unaofanya nyimbo zake kuwa na mtiririko wa kishairi, na (b) muundo wa simulizi wenye kufanya hadithi fupifupi. Kaida hizi mbili za muundo zinajadiliwa kwa kutumia nyimbo mbili, nazo ni *Zuwena* na *Dunia Imani Imekwisha*. Nyimbo hizi zinathibitisha utamu unaotokana na ruwaza za beti, misitari, na vishazi, kuwa muhutasari wa tajriba ya watu, na matumizi ya lugha ya masimulizi ya visa na mikasa. Japo hadithi katika nyimbo ni fupi lakini zina sehemu zote za simulizi nazo ni: (a) ikisiri, (b) mwongozo, (c) mgogoro, (d) utatuzi, (e) tathmini. Nyimbo za Marijani Rajabu zinawakilisha tajriba ya watu wengi wa Tanzania na harakati za mwananchi wa kawaida kupambana na changamoto mbalimbali za maisha.

23. Cristina Nicolini (Rome)

Of Madness and Sagacity: Masks in Luigi Pirandello's & Penina Muhando's Plays

This research, which stems from the challenge of translating Pirandello's plays into Swahili, is aimed to open up a polylogue between Italian and Swahili literature. Therefore, in searching for connections between Luigi Pirandello's and Penina Muhando's plays, this paper will explore multiple masks engaged in a reciprocal dialogue among the following six selected plays: *Enrico IV* ('Henry IV', Pirandello, 1921); *Così è, Se vi pare* ('It is so, If you think so!', Pirandello 1917); *Il Berretto a Sonagli* ('Cap and bells', Pirandello 1916); *Pambo* ('Decoration', Muhando 1975); *Nguzo mama* ('The Mother Pillar', Muhando 1982); and *Lina ubani* ('An Antidote to Rot', Muhando 1984).

24.Nathan Ogechi (Eldoret)

To Collaborate or to Partner?": Research and Language Description of Indigenous Languages in Kenya

The proposed paper attempts to address the challenges of describing grammars of African languages (documented or otherwise) in Kenya against the backdrop of the colonial ideology. Until the advent of European imperialism, Kiswahili was the only African language whose rich culture, poetry, was documented using the Arabic script. Subsequently, the description of Kenyan indigenous languages, including Kiswahili, was pioneered by the Christian missionaries using the Latin script. Hence, non-native speakers of African languages took a lead in the identification of what constituted a language, its dialects, their names and orthographies (Prah 1998, Kadanya 2020) thus bringing to fore the question on whether or not there was splitting and lumping of languages (Heine & Nurse 2000), and the acceptance and reliability of the grammars (Ogechi, Ngala-Oduor & Iribemwangi 2012, Akumbu 2020). The non-coordinated efforts have led to the continual split of languages, on one hand, and the launch of harmonization and standardization of Kenyan languages and their orthographies. While acknowledging the trailblazing role of the missionaries and their European sponsors in language description, the paper calls for a bottom-up collaborative approach in describing African languages. Through a historical-sociolinguistic approach, the paper will interrogate the language description (and translation) efforts by bodies such as SIL, Bible Translation and Literacy, Kenya Institute of Curriculum Development and CASAS while taking cognizance of the Constitution of Kenya 2010 which officially elevated Kiswahili to a co-official language and the “exclusion” of universities and research institutions.

25. Shani Omari (Dar es Salaam)

Mchango wa Wasanii wa Kike wa Muziki wa Hip Hop Nchini Tanzania

Wasanii wa kike wa muziki wa Hip Hop nchini Tanzania, tangu kuanza kwa muziki huu nchini humo mnamo miaka ya 1980, wamekuwa na mchango mkubwa katika sanaa hiyo. Miongoni mwa wasanii hao ni Happiness Thadei Pella (Sister P), Nakaaya Sumari, Witness Mwaijaga Sigbjorn (Witness Kibonge Mwepec), Zainab Lipangile (Zay B), Florence Kasela (Dataz), Fredinah Peyton (Rah P), Chiku Keto na Da Joh. Wengine ni Rosary Iwole (Rosa Ree), Frida Amani (Queen FiFi), na Claudia Lubao (Chemical). Ushiriki wao katika muziki huu ulizidi kuifanya jamii kulegeza mtazamo kwamba muziki ni uhuni na badala yake kubaini kuwa ni ajira na chanzo cha kipato. Mitindo yao ya ‘uchanaji’ na maudhui ya nyimbo zao yamewavutia wengi na kuleta ushindani mkubwa katika tasnia nzima ya muziki huo. Makala hii inalenga kuchunguza maudhui ya nyimbo za wasanii wa kike wa Hip Hop yanavyochangia katika kutoa maarifa mbalimbali kwa jamii. Wasanii hao ni wengi haitawezekana kushughulika nao wote. Kwa umahususi makala itachunguza nyimbo za wasanii wawili (Dataz na Chemical). Uteuzi wa sampuli ya wasanii hawa ni wa kinasibu tu. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kufanya mahojiano na wasanii husika na kuchambua maudhui ya nyimbo zao. Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba nyimbo zao zinazungumzia masuala mbalimbali yakiwemo ya kisiasa, uchumi, utamaduni na yale yahasuyo vijana wenyewe

26. Teresa Poeta, Hannah Gibson, Fridah Kanana Erastus and Lutz Marten (Essex / SOAS & Nairobi/Munich)

**Swahili Variation Documented Through Time:
A Reflection on the Descriptions and Their Authors**

This talk presents a systematic overview of the documentation of Swahili dialects in early linguistic descriptions. Mention of dialectal variation is found in language handbooks from as early as the the end of the 19th century (e.g. Steere 1870), as well as in Ashton's (1947) *Swahili Grammar (including Intonation)* – to this day a key reference point in Swahili linguistics. Dedicated publications documenting specific dialects and varieties spoken along the coast of Kenya and Tanzania such as Kivumba, Kimvita and Kingao were also published from the early 20th century onwards (e.g. Sacleux 1909, Stigand 1915, Lambert 1957).

In this talk, we explore how Swahili variation was captured, by whom and why in these early descriptions. We are particularly interested in accounts of morphosyntactic variation, which has received less attention in comparison to phonological and lexical differences. In reflecting on and reviewing this body of work, we consider issues of power, authorship and voice, and discuss the historical and sociocultural factors which influenced which dialects received scholarly attention and why. We focus on the background and motivations of the authors and their relationships to the speakers of the dialects. We observe that in a large proportion of the work from the late 19th and early 20th Century, the voices and identities of European linguists and missionaries are foregrounded, while contributions of Swahili speakers remain largely unmentioned and unrecognized.

27. Annachiara Raia (Leiden)

Reconfiguring a Swahili Modern Library from the Indian Ocean Island of Lamu

Despite the relatively abundant Swahili-language collections of manuscripts and print materials in East Africa and Europe, it has nevertheless also been highlighted how the local collections housed in university libraries or private households in East Africa are in fact, fragmented, difficult to access and often endangered, and/or on the verge of disappearing (Kresse and Vierke 2022). The private library of living poet and imam Ustadh Mau from the Indian Ocean island of Lamu (Kenya) can be regarded as a representative contemporary example: a unique yet overlooked and at-risk site where local epistemologies composed in the regional language variety of kiamu are still collected and produced. In 2022, the Ustadh Mau Digital Archive (UMADA) was among the 29 international cultural preservation projects that received a grant from the Modern Endangered Archives Program from UCLA Library. In this paper, I will present the collection, made of roughly two thousand fragile materials that a team in Lamu aims to document and digitize, among which: handwritten manuscript poetry in Arabic script, letters, printed texts, biographical photos and audio cassettes of his Friday sermons, delivered since 1986. I will also discuss the challenges on how to enhance this archive accessibility and findability through accurate metadata that adds on standards metadata categories adding hitherto neglected "southern notions". Providing these materials through digitization, accurate metadata and OA platforms opens them up for new audiences and readers and will enhance new research into overlooked local productions and literary canons from colonial and postcolonial contemporary Kenya.

28. Ute Reuster-Jahn (Hamburg)

Laiti Ningelijua - The Autobiography of Nicco ye Mbajo, Popular Artist in Tanzania (1950-2021)

This paper is concerned with the autobiography of the Tanzanian popular artist Nicco ye Mbajo (1950-2021), published in 2020 and entitled *Laiti ningelijua* ('If I had known'). As writer and illustrator of books, cartoonist, editor and co-founder of the popular magazine *SANI* (established in 1978) and later *Mcheshi*, Mbajo belonged to the young cultural producers who significantly shaped early popular print culture in Tanzania. He was also a talented musician, establishing a dance band in the 1970s and later becoming a well-known choir leader in Dar es Salaam. His autobiography offers a subjective view of the various, often contradictory cultural currents and social struggles related to the political project of decolonisation and "national culture" in post-independence Tanzania. He had to navigate, and in fact was often torn between his Christian faith and affiliation with the Lutheran church, employment, patriotism and socialist ideas, his creativity and fascination with modern and transnational forms of art and culture, family obligations and the pursuit of personal happiness. Based on an analysis of his autobiography, interviews and personal communication, I flesh out some of these conflicts and show how they shaped the author's career and personal life – and those of the emerging urban and popular cultural elite more broadly - in the years following Tanzanian independence.

29. Izabela Romańczuk (Warsaw)

Vamps and Victims? A Renewed Attempt to Characterise Women in Swahili Literature

Swahili literature has been the subject of numerous literary studies and analyses, as well as the focus of interdisciplinary research looking at linguistic, sociological or philosophical issues. The vast majority of research has focused, and continues to focus, on androtexts, with women's work remaining highly marginalised.

A controversial conclusion on the insufficient state of research on women's writing is presented by Elena Bertoncini-Zúbková in *Vamps and Victims: Women in modern Swahili literature* (1996). In her work, the author focuses on female characters in the novels of well-known Tanzanian writers and does not include a single text written by a woman. This choice, she argues, is due to the fact that a handful of female writers were not interested in women's problems. Moreover, the researcher claims that, a "true feminist approach" to the situation of women was presented by male writers, and it is to them that we owe the creation of memorable female characters in Kiswahili literature (Bertoncini-Zúbková 1996: 9-10). The statements raise the question of the feminist paradigm that the researcher had in mind but refrained from presenting. What is a "true feminist approach"? In my view, the theses that shape the anthology of *Vamps and Victims...*, can be described as exclusionary practices (characterised by Florence Stratton in 1994), that are grounded in [un]conscious androcentrism and Eurocentrism in the study of women's literature from the Global South. Ultimately they contribute to the marginalisation of women's work and isolate it from the Swahili literary and intellectual tradition, including the feminist discourse created within it.

In my presentation, I will take a selection of Swahili novels by Tanzanian women writers from late twentieth-century from authors such as Lucy Nyasulu, Zainab Mwanga and Zainab Burhani, to verify Elena Bertoncini-Zúbková's statements. Instead of trying to fit the narratives into a rigid framework of a true feminist approach, I will try to take a critical look at the writers' attempts to shape locally oriented emancipatory and feminist discourses.

Key words: women, feminism, female writers, Swahili novel, Tanzania

30. Ding Ruilin (Beijing)

“Joram Kiango” in Reality: Reconsidering Ben Mtobwa’s Contribution to Swahili Popular Literature

Ben Mtobwa is a well-known and prolific Tanzanian novelist who has written a number of detective novels that have gained wide popularity among readers in East Africa. However, for a long time there has been a strict division between popular and serious literature in Swahili scholarship, and popular literature has often been undervalued, even considered by some scholars as worthless written works. As a result, Mtobwa's works have also been labeled as 'insignificant' and 'for pleasure only'. Nevertheless, Mtobwa has made a significant contribution to the transformation and development of Swahili popular literature, and his popular novels have richer connotations, such as criticism of social darkness and conveying political messages which are inextricably linked to Tanzanian society and a broader movement of freedom struggle in Africa. It was under his influence that popular fiction of the certain period underwent further development and took on the responsibility of serious literature to some extent. In addition, Mtobwa was also a famous publisher and facilitated the publication of Swahili popular literature. In this paper, I will discuss Mtobwa’s contribution both in the 'literary' and 'extra-literary' spaces, analyzing his popular novels in terms of their social-critical discursive construction and politicization, as well as the contribution he made to the development of Swahili popular literature as a publisher.

Keywords: Ben Mtobwa; Swahili popular literature; social-critical discourse construction; politicization of popular literature

31. Kenneth Simala (Kakamega)

Liyongo, Swahili Poetry and Public Intellectualism

This paper discusses the role of Fumo Liyongo as a public intellectual in the evolution of the Swahili public sphere. It examines the relationship between Swahili poetry and the public sphere as it is addressed in Liyongo's literary works and how he used his position as a public intellectual to engage in a struggle against dominant discourses and ways of seeing. Situating Liyongo in his material and historical contexts, the paper offers an explanation of why Swahili poets are well situated as public intellectuals to fulfill this social function. In attending closely to the role of the public sphere in Liyongo poetry, the paper offers a new lens through which to understand some of his significant poems. It argues that poetry has been an ideal site for building and maintaining a Swahili public sphere.

32. Kadara Swaleh (Berlin)

Mohamed Ali (Jicho Pevu): Mwanahabari, Mwanasiasa na Mwanaharakati wa Lugha ya Kiswahili, Kenya.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa ya Kenya na vilevile ni lugha rasmi. Takriban shuhuli zote za kiserikali kama vile utawala, elimu na biashara zinaendeshwa kwa Kiingereza. Asiyejua lugha ya Kiingereza hudharauliwa na kudhaniwa kuwa ni mpumbavu. Kwenye shule za kitaifa, Kiswahili huzungumzwa wakati wa somo la Kiswahili peke yake. Kwa miaka mingi wanafunzi wamekuwa wakipewa adhabu au kufedheheshwa wanapozungumza Kiswahili shuleni. Miongoni mwa orodha ya uhalifu wa wanafunzi shuleni ni kuzungumza Kiswahili (“Swahili speakers”) kama vile kuchelewa shule (late comers), kutoenda shule (list of absentees), ama kufanya fujo darasani (noise makers). Tabia hii imeleta athari kwenye nyanja mabalimbali za maisha. Hivi karibuni mamia ya vijana kutuko mji wa Mombasa walinyimwa kazi ya ubaharia (sailors) na Wizara ya Bandari kwa sababu kiwango chao cha Kiingereza hakiridhishi. Taasisi nyengine iliyoathirika ni bunge la kitaifa (National Assembly) ambapo wajumbe wana hiyari ya kuzungumza Kiingereza ama Kiswahili. Karibu wajumbe wote wanatumia Kiingereza bungeni na wale ambao hawajui hunyamaza kimya kwa sababu kutumia Kiswahili ni kama kujiaibisha.

Mohamed Ali alizaliwa mwaka 1979 mjini Isiolo karibu na mpaka wa Kenya na Ethiopia. Alianza kazi kama mwanahabari kwa lugha ya Kiswahili kwenye runinga ya KTN. Alipata umaarufu zaidi alipokuwa kinara wa kipindi cha investigative journalism kinachoitwa Jicho Pevu (Bird’s-eye View). Kwenye kipindi hiki alifichua siri na kashfa nyingi za serikali. Alipendwa sana na watu na akapata umaarufu mpaka sauti yake na utangazaji wake ukawa ni miongi mwa “ring tones” ya Wa-Kenya wengi. Vilevile, aliingia Bunge la kitaifa kwa mara ya kwanza 2013 kama independent candidate akiwakilisha eneo la Ki-fahari la Nyali, mjini Mombasa. Huko bungeni, Mohamed Ali aliamua kuzungumza Kiswahili kwenye mijala yote ingawa Kiingereza chake ni safi kabisa. Hatua hii ilizidi kuhalalisha utumizi wa Kiswahili bungeni. Pia imewapa ujasiri wajumbe wengine kutumia Kiswahili. Jambo hili limemfanya Mohamed Ali atambulike kama miongoni mwa MASHUJAA wa Kiswahili nchini Kenya.

Wasilisho hili linaangazia juhudi ya Mohamed Ali katika kupigania haki za wanjunge akiwa bungeni na nje barabarani kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama silaha. Utafiti huu unamulika mradi wa Kitaifa wa Miundombinu wa Reli ya Kisasa, Standard Gauge Railway (SGR), unaofadhiliwa na Serikali ya Uchina kupitia mradi wa Belt and Road Initiative (BRI). Reli hii inayotoka Mombasa kwenda Nairobi mpaka Naivasha imewaathiri na kuwadhalilisha wafanyakazi na wanabiashara wa Mombasa na kufanya mji wa Mombasa uwe kama gofu (abandoned city).

Baada ya uchunguzi wa kina, ilithibiti kwamba wakuu wa serikali na mawakala wao walileta sheria potofu (kwa maslaha binafsi) kama “marufuku ya malori kubeba mizigo” na kuipatia reli ukiritimba (monopoly) wa kusafirisha shehena zote. Wasilisho hili linatazama namna gani Mohamed Ali na wenzake walisimama kidete bungeni, mahakamani, na barabarani kupambana na madhalimu.

33.Duncan Tarrant (Bayreuth)

The Poetry of Nassor Hilal: The Ever-pressing Burden of Time

Nassor Hilal Kharusi is a Zanzibari poet, writer and philosopher, who has published four anthologies of poetry to date. In this presentation I will give examples of some of his work focussing on two of his anthologies – *Siku Zapishana* (2018) and the unpublished *Nasaha*. Of particular interest for this paper are the poems which use new or unconventional meters, and those which demonstrate the poet's philosophical perspectives on time, people and the world.

34. Rayya Timammy (Nairobi)

Mtunzi wa Kiswahili kama Mshairi na Mhifadhi wa Maarifa ya Kijamii: Kifani cha Utenzi wa Kikuba wa Mahamoud Ahmed

Kazi hii inachangia uelewa na ukuaji wa ushairi wa Kiswahili kwa kuangazia mmoja katika washairi wa kiswahili wa kijadi Mahamoud Ahmed na kwa jina la lakabu MAU ambaye licha ya kuchangia kazi nyingi za ushairi kwa kipindi cha miongo minne hivi hajafanyiwa utafiti mwingi na hivyo kupuuzwa na watafiti. Tunalenga kuonyesha mchango wake wa kisanaa na namna mchango huo unavyoathiri maendeleo na mitazamo ya jamii ya Waswahili. Katika kufanya hivi tumetumia mtazamo wa kinadharia wa kiethnomethodolojia unaohusishwa sana na mawazo ya Garfinkel (1967) ambao unatumia maarifa na taratibu za jamii kuihakiki. Data ya kazi hii ilipatikana maktabani tuliposoma kazi za mshairi huyu na kuzifanyia tathmini na uchunguzi kwa misingi ya desturi za Kiswahili huku zikiwa zimefungamana na dini ya Kiislamu. Imebainika katika uchunguzi huu kuwa kazi za Mau hasa Kikuba zinaelimisha vijana kwa misingi ya dini ya Kiislamu na utamaduni wa Waswahili na kwa wakati huo ikidara athari hasi zinazopotosha maendeleo chanya ya jamii hasa yanayofungamana na ndoa za Waswahili.

35. Katrina Daly Thompson (Madison)

Evolving Swahili Islamic Marital Advice (1932-2020)

In this presentation, I will share preliminary findings from my ongoing analysis of almost ninety years of Swahili-language marital advice booklets that address issues of weddings, marriage, sexuality, and divorce. I will discuss how the content, style, authorship, and format of such pamphlets have evolved due to various factors, including changes in societal attitudes and values, technological advancements, and the influence of various cultural and religious trends. In addition, I will discuss how the written advice, aimed chiefly at Muslim men, is both similar to and differs from Muslim women's oral advice I examined in earlier ethnographic research in Zanzibar.

36. Martin Walsh (Arusha)

Living by the Sea: Lexical Evidence for Early Swahili Adaption and Innovation.

This paper will focus on the creativity of Swahili -- the local voices and histories embedded in the lexicon -- in different lexical fields relating to living by and from the sea. Swahili has a rich vocabulary of terms for marine resources and the gendered technologies of foraging, fishing and sailing. Etymological research provides insights into the ways in which the early Swahili adapted to marine environments and their exploitation, developing new knowledge and innovating practice as they did so. As well as presenting some of the evidence for this and its relevance to the debate about when and to what extent the Swahili became "maritime", I will discuss the methodological issues raised by cross-dialectal comparison and historical reconstruction in Swahili and related Sabaki languages, especially Comorian. I will also highlight the many gaps in our knowledge and the potential for participatory research in Swahili lexicography and dialectology, which deserve to be more highly valued than they are.

37. Sheila Wandera (Laikipia)

Usasaleo katika Ufundishaji wa Mashairi ya Kisasa: Matumizi ya Mashujaa wa Kisasa

Postmodernism in the teaching of Modern Swahili Poetry: Upcoming Mashujaa Works

Ushairi ni kitengo muhimu katika fasihi ya Kiswahili. Kuna kozi ya Ushairi wa Kiswahili inayofunzwa katika vyuo vikuu nchini Kenya katika idara za Kiswahili au zinazohusiana na Kiswahili. Kozi hii inahusisha mashairi ya kale na/ au mashairi ya kisasa. Mashairi ya Kisasa yanapofundishwa huangaliwa katika vitengo viwili; cha kimapokeo na cha kimapinduzi. Aghalabu, mashairi yanayozingatiwa ni yale yaliyotungwa na waandishi tajika na kuchapishwa katika diwani mbalimbali. Mashairi haya ni mazuri lakini katika enzi hii ya usasa leo kuna haja ya kushughulikia wasanii wanaoibuka miongoni mwetu, ambao ingawa hawajachapisha, wametunga na wanaendelea kutunga mashairi yanayoendana na wakati huu. Hawa wanatambuliwa na wanajamii, na wanapatikana katika sherehe mbalimbali za kijamii, katika vipindi vya redio, katika magazeti na hata miongoni mwa magwiji wa Kiswahili. Tunapofunza kozi hii ya ushairi, tukitenga muda wa kusikiza mashairi haya redioni, kuyasoma magazetini, kuwatembelea wasanii hawa, au hata kuwaalika chuoni tutapata fursa nzuri ya kujifunza mengi kutokana na tungo hizi, na pia kuwapa motisha wanafunzi tunaowafunza kuwa watunzi baadaye. Katika enzi hii ya dijitali, pia tunaweza kuingiliana nao kupitia mitandao mbalimbali. Hali hii itafinyanga upya ufundishaji wa taaluma ya ushairi katika vyuo wetu kupitia mashujaa miongoni mwetu. Makala hii basi itachunguza mchango wa mashujaa wa ushairi miongoni mwa jamii zetu katika kuufinyanga upya ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili kati vyuo vikuu nchini mwetu. Nadharia ya usasaleo itatumikizwa katika kuhakiki ufinyanzi upya wa tungo hizi za wasanii. Ni katika mwelekeo huu ambapo ushairi wa Kiswahili utaendelezwa, huku ukipewa pumzi mpya na wasanii na wapenzi wa Kiswahili kwa jumla. Izingatiwe kuwa Kiswahili sasa ni lugha ya umataifa, na sharti itazamwe kwa mapana na marefu yake.